JUSTICE WITH CHILDREN
www.justicewithchildren.org

# MAKUBALIANO KWENYE NGAZI YA DUNIA KUHUSU HAKI KWA WATOTO

20 Novemba 2021

Mkutano wa Dunia kuhusu Haki kwa Watoto wa 2021;

***Ilikusanya*** zaidi ya washiriki 4800 wa umri wa miaka mbalimbali kutoka zaidi ya inchi 100 kuanzia tarehe 15 mpaka 20 Novemba 2021 kwa njia ya mtandao, na mada "Kuhakikisha watoto wote wanapata haki: hatua kuhusu mifumo ya haki isiyo bagua ao kutenga watu";

***Ilitayarishwa*** na (Mupango wa Kimataifa wa Haki kwa Watoto) (muungano wa Terre des hommes, Penal Reform International, Chama cha Kimataifa cha Vijana na Waamuzi na Wanasheria wa Familia pamoja na Kituo cha Kimataifa cha Haki za Mtoto) na ilifanyika Mahakamakuu ya Haki ya Meksiko kwa musaada wa kiufundi kutoka Shirika la Hazina la Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Watoto (UNICEF), kupitia Ofisi ya Mwakilishi wa kipekee wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu Unyanyasaji kwa Watoto, Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayo husiana na Madawa ya Kulevya na makosa kinyume na sheria,Ofisi yaMusimamizi Mkuuwa Umoja wa Mataifa kuhusu haki za binadamu, Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo, na Wasuluhishi kwa ajili ya jamii zenye amani, haki na kushirikisha watu wote; chini ya usimamizi wa Baraza la Ulaya na Bunge la Ulaya; kwa musaada wa bila malipo kutoka kwa Baker McKenzie; na muchango kutoka kwa Kamati ya Kisayansi, Kamati ya Heshima, Kikundi cha Ushauri cha Mtoto na Vijana, na mikutano ya maandalizi ya kwenye ngazi ya kanda na taifa ya Mkutano wa Dunia;

***Ilizibitisha tena***makubaliano inayo faa kwa ajili ya kuhimiza, kulinda na kutimiza haki za watoto ambazo zina patikana katika Makubaliano wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Mtoto na kanuni zingine za kimataifa kuhusiana na haki za mtoto;

***Ilikumbusha tena*** makubaliano ambayo ilitayarishwa katika Tangazo ya Paris (Ufaransa, Mei 2018), Tangazo ya Geneva (Uswisi, Januari 2015), na Tangazo ya Lima (Peru, Novemba 2009) ya Mikutano ya Dunia ambazo zililenga mada kuhusu haki kwa watoto. , haki ya kulipwa, na kuimarisha mifumo ya haki ya mtoto;

***Kusaidia*** mapendekezo na matendo iliyo tolewa na kutajwa katika Wito wa kimataifa *kwa ajili ya haki kwa watoto*(Septemba 2019) na Wasuluhishi kwa ajili ya jamii zenye amani, haki na kushirikisha watu wote  kuhusiana na shaba ya 16 ya maendeleo ya kudumu, iliyo andaliwa na kupendekezwa na kundi tofauti ya mashirika ya kiserkali na mashirika ya kiraia na vituo vya masomo kwenye ngazi ya kimataifa, kanda na ya kitaifa;

***Ilitambua*** haja ya kusisitiza tena mapendekezo iliyo tolewa na watoto na vijana katika hotuba yao kwenye Mkutano wa Dunia iliyo pita (Ufaransa, Mei 2018); umuhimu wa mwongozo iliyo tolewa katika *Utafiti wa Umoja wa Mataifa kuhusu watoto waliyo imwa uhuru* (Novemba 2019); vinyume vya ugonjwa wa corona (COVID-19) kwenye kuzuwia haki kwa watoto vilivyo tajwa katika *Mufano kwa kifupi wa Umoja wa Mataifa (ONU): Vinyume ya COVID-19 kwa watoto* (Aprili 2020) na *tamko ya kiufundi ya Interagency: COVID-19 na Watoto kuimwa uhuru wao* (Aprili 2020); somo kutoka shirika la UNICEF kuhusu *Kupata Haki kwa Watoto katika kipindi cha COVID-19: Mafunzo kutoka kwenye Mkutano* (Desemba 2020); na makubaliano kuhusu watoto iliyo fanyika na ma rais wa nchi na serkali, mawaziri, na wakilishi wa inchi wanamemba wa Umoja wa Mataifa katika makubaliano ya Kyoto kuhusu Kuzuwia makosa kinyume ya sheria, Haki kuhusiana na makosa kinyume na sheria na Kanuni za sheria (Japani, Machi 2021) kwenye  mkutano wa kumi na ine wa Umoja wa Mataifa kuhusu Kuzuwia makosa kinyume na sheria na Haki kuhusu vitendo kinyume na sheria;

***Ina gundua*** mambo *ifuatayo:*

1. Kwamba ijapokuwa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto (CRC) haitaji maneno ya kipekee kupata haki ao suluhisho, hiyo neno inapatikana katika makubaliano, ikiwemo kanuni za mapendekezo bora; haki ya watoto kupokeya habari, kutowa maoni yao, na kusikilizwa; haki ya kulindwa na aina zote za unyanyasaji; haki, ulinzi na kanuni za kufwata kuhusu watoto wenye kupatikana katika hali ya mizozo na wenye kupelekwa mbele ya sheria; na hatua zinato patikana kuhusiana na kuimwa uhuru na ikiwemo kutunza na kuwezesha watoto wahanga kushiriki tena katika mambo mbalimbali;

2. Kwamba Makubaliano kwenye ngazi ya dunia ya Haki za Binadamu na Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki za Kiraia na Kisiasa, katika mambo mengine, zina tekelezwa pia kwa usawa kwa watoto wote, na kudai kwamba mtu yeyote ambaye haki ao uhuru wake unakiukwa iko na haki ya kupata suluhisho inayo faa, na kwamba sheria hiyo inapashwa kuwekwa na mahakama yenye uwezo, uongozi, ao mamulaka za kutunga sheria, ao na mamulaka yoyote ile yenye uwezo inayoto lewa na chombo cha kisheria ya inchi;

3. Kwamba kanuni ya kutobaguwa ni nguzo kubwa ya Makubaliano kuhusu haki za Mtoto (CRC) na inatumika kama musingi wa vyombo vingi vya kisheria vya kimataifa, kanda na ya kitaifa;

4. Kwamba  Inchi  Wanamemba kwenye  Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa  zilikubaliana kuhusu  kupata haki sawa sawa  kama  haki ya musingi, ikiwa ni pamoja na watoto, na kwamba kuhakikisha kutowa haki sawa sawa kwa wote na kukomesha unyanyasaji zidi ya watoto ni mambo mihimu ya Ajenda ya 2030 ya Développement durable, hasa Lengo ya 16;

5. Kwamba watoto wanageuka wahanga kwa sababu ya mapungufu ya jamii, ikiwa ni pamoja na aina mbalimbali za unyanyasaji ambazo zina fanywa kwao ndani na inje ya hali ya kisheria, ambao inakuwa na vinyume mingi kwa watoto waliyo tengwa na kuzuwia juhudi za kuzuwia na kupambana na hali na hatari ambayo inasababisha watoto kupelekwa mbele ya sheria, iwe kama muhanga/aliye pitia hali ya uhanga, anaye fatiliwa ao muhukumiwa, shahidi, muchanganyiko hali zote, ao katika hali yoyote ile;

6. Kwamba janga ya ugonwa wa corona (COVID-19) iliongeza ukosefu wa usawa wenye uko ndani ya jamii na kuzoofisha zaidi ao kupunguza nguvu yote ya mifumo ya haki na ulinzi wa mtoto ambazo ziko tayari ni zaifu, na kwamba iyi matatizo zina ongezeka zaidi na maelfu ya mizozo zingine za kisasa na zinazo endelea, ikiwa ni pamoja na mizozo ya mabadiliko ya hali ya hewa na ya kimazingira, mizozo ya arzi na ya kisiasa, na mizozo ya kisilaha, mizozo ya kiuchumi, na hali zingine za zarura ya kibinadamu, ambazo zinahitaji suluhisho na mifumo inayo faa na mbinu zinazo wezesha watoto wote kuendelea napata haki;

7. Kwamba ulimwengu ulizidi kushuhudia watoto na vijana waliyo wezeshwa wakiwa mstari wa mbele katika harakati za kitaifa na kimataifa zinazo dai haki za kijamii, za kijinsia, rangi, hali ya hewa, na kisiasa,wakati wa maongezi mbalimbali na kuweza kusabaisha marekebisho ya mfumo wa haki;

8. Kwamba kukosekana kwa ubaguzi na ukosefu wa usawa katika mfumo wa haki ya mtoto na katika kutowa haki ilikuwa na faida kwa watoto wote, bila kujali wao ni nani, wanatoka wapi ao hali gani yenye wana patikana amo;

9. Kwamba watoto wanao pelekwa mbele ya sheria wako na haki sawa na mtoto yeyote ule mwingine, jambo ambayo inahitaji heshima na usawa na ulinzi wao wa haki na maisha bora, kwa kuzingatia mapungufu na mahitaji ya kipekee ya kila mtoto na kutambuwa uwezo wao siku kabla ya siku;

10. Kwamba ni muhimu kwa mifumo inayo simamia mambo kuhusinana na haki, ukingo na maisha bora kwa wa mtoto, ulinzi wa kijamii, elimu, na huduma ya afya, miongoni mwa mambo mengine, kufwata uongozi na ushirikiano wa mambo mbalimbali ili kushurulikia muzuri kesi zinazo husisha watoto wanao pelekwa mbele ya sheria kwa namna yoyote;

***Inaheshimia*** sauti zifwatazo za watoto na vijana zilizo kusanywa na Kikundi cha Ushauri cha Watoto na Vijana cha Mkutano wa Dunia:

11. Sisi ni kundi ya watoto na vijana ambao wana husika na haki za watoto kwa kuwasiliana na mifumo ya sheria, hasa kwa sababu wengi kati yetu tulitumia iyi mifumo moja kwa moja, na kulingana na matokeo yenye tuligundua wenyewe, tunazani kwamba:

    a. Ubaguzi kati ya vizazi na ukosefu wa usawa wa kiuchumi ni sababu kubwa za watoto wanao pelekwa mbele ya sheria;

    b. Watoto wanao pelekwa mbele ya sheria wanapata aina mingi ya matatizo, zikiwemo unyanyasaji wa nyumbani, kutengwa kwenye elimu, jambo ambayo inaweza kuwa na vinyume kubwa ku afya ya akili ya watoto;

c. Mifumo ya sheria haitangulizi mbele haki za watoto, jambo ambayo ina sababisha watoto mingi kujisikia kuumizwa, kupuuziwa, na kufazaika na mfumo wa haki;

d. Mara mingi mifumo ya haki vitendo ya nyuma sheria zinazingatia azabu na hukumu kuliko kurekebisha na kurudisha amani;

12. Tunaamini kwamba watoto ni raia wa leo na viongozi wa kesho, na tunaomba watu wazima watambue hiyo na wawezeshe watoto kujuwa haki zao;

13. Ili kuleta mabadiliko ya kweli kwa watoto wanao pelekwa mbele ya sheria, tunaomba serkali na mashirika ya kiraia kufanya kazi pamoja na watoto na vijana ili kuhakikisha kwamba haki za watoto wote, kama vile zilizo tayarishwa katika sheria za kimataifa, zinatimizwa kwa kila mtoto duniani kote.

14. Hasa, tunaomba:

a. Watoto wote wapewe fursa sawa ya kupata haki kwa njia ya kushirikisha kila mtu na isiyo bagua kwa sababu yoyote ile;

b. Watoto wapewe uhuru wa kutowa maoni yao na maoni yao ichukuliwe kwa kwa makini;

c. Watoto wawezeshwe kufanya maamuzi kuhusu maisha yao wenyewe, na kwamba waweze kupokea musaada wa kutosha kutoka kwa watu wazima;

d. Watoto wapewe habari na maelekezo wa namna bora ya kushurulikia hali ya kutokuwa na uhakika na wakati wa shida, kama vile janga la sasa;

e. Watoto ambao wanapelekwa mbele ya sheria wanatendewa kama watu, ambapo haki zao zina heshimiwa, na ambayo inachukua mbinu bora kwa ajili ya afya yao ya akili na maisha bora;

f. Vijana ambao wanapelekwa mbele ya sheria ambao "wako na umri yenye inakaribia" ya watoto wahukumiwe kama watoto;

g. Watoto na vijana wanapewa fursa ya kujifunza kuhusu na kushiriki katika hatua za kurekebisha;

h. Watoto na vijana wasaidiwe kuomba haki zao, jambo ambayo ni muhimu katika kuamini tena mifumo ya haki;

15. Tuko na uhakika kwamba haki ya kweli kwa watoto na pamoja na watoto inaweza kupatikana wakati watoto wote wanachukuliwa sawa sawa na kupewa fursa za kufanya kazi kwa kushirikiana na watu wazima ili kutimiza ahadi za haki za binadamu;

***Kwa hivyo, sisi kama watayarishaji, washirika na washiriki kwenye Mkutano wa Dunia, kwa pamoja tunatowa wito*** kwa watowa misaada wote wanao husika, ikiwemo inchi na mashirika ya kiraia, zipate:

## Kutekeleza Haki na Watoto kwa njia inayo faa, leo na kesho

16. Kufanya kazi mukono kwa mukono, kama watoto na watu wazima ili kuwezesha watoto duniani kote kupata haki bila ubaguzi na kwa usawa kwa namna ambayo watoto wana chukuliwa kama wajuzi wa mambo na washiriki wakuu katika mbinu hizo za mabadiliko bora, ikiwemo kanuni za haki ya mtoto na kuwezeshwa kupata haki, kutunga na kurekebisha mifumo ya kiesheria, matumizi ya mifumo na namna ya kuweka hatua za kisheria, uwezo- kuelimisha watendaji wenye kuhusika; na kuimarisha utowaji kwa watu wanao husika, jamii na zingine jamii mbalimbali;

17. Kuboresha mazingira inayo wezesha watoto kuwa kama wenye haki ili wapate kutumika kama waleta mabadiliko, na kuongeza sauti za leo na siku zijazo, kutowa maelekezo inayo jali watoto yenye kuzingatiya jinsia, na ulemavu na habari kuhusu sheria na hatua za kisheria, kuboresha usikiliku kwa watu ndani ya jamii kuhusu usawa kati ya haki za watoto kwa watoto na watu wazima, kuendelesha utowaji wa habari zinazo lenga mtoto kwa njia ambayo ni bora zaidi kwa kufikia watoto, na kuhakikisha mbinu ambazo zinashirikisha na kuwezesha watoto kushirikia haijalishi hali zao za maisha, ikiwemo na watoto wote wanao pelekwa mbele ya sheria;

18. Kushurtisha watoto washirikishwe katika sheria na kutumia iyi sheria ili kuhakikisha watoto wana shiriki katika mazungumuzo, kuliko kuhimiza tu ushirikisho wa watoto na kuhakikisha watoto wana kuwa mada katika mazungumuzo na maamuzi, hasa kwa makundi ya watoto wanao pelekwa mbele ya sheria ambao mara mingi hawashirikishwi katika mazungumuzo kwa sababu ya ubaguzi, kutengwa, mazingira nguvu ao hali mubaya yenye wanapatikana amo;

## Kuwezesha watoto wote wapata haki bila ubaguzi

19. Weka mambo ya ukosefu wa usawa na ubaguzi katika mazungumuzo na marekebisho yoyote kuhusu haki ya mtoto, na kuanzisha njia za kuleta suluhisho kwa kumesha vitendo ya ubaguzi kwa kila mtoto kwa njia yoyote ile anaye pelekwa mbele ya sheria, kwa namna ya kuepuka hali mubaya na alama ya kurauliwa;

20. Kuhakikisha watoto wote wanapata haki sawa sawa, hasa wale wenye kutokeya katika makundi iliyo tengwa, kwa namna ambayo inaambatana muzuri na haki kuhusu vitendo ya kinyume ya sheria, ya kiraia, kiutawala, ya kitamaduni/kimila, ya mpito na ya kijamii;

21. Kuendelesha na kutumia vyombo, kanuni na hatua za sheria kulingana na umri, ulemavu, jinsia, na mahitaji na hakikwa watoto wote ambao wanapelekwa mbele ya sheria ambazo zinaambatana na kulingana na sayansi kuhusu akili, kukomala na tabia;

22. Kuweka hatua ambazo zinaheshimu na kutatuwa tofauti za kitamaduni na luga ya kila mtoto ambaye anapelekwa mbele ya sheria;

23. Kuanzisha huduma za kijamii na hatua ambazo hazitumiyi njia ya mahakama ambazo zina wekwa muzuri sana ndani ya jamii zenyewe na zenye watoto wote duniani wanaweza kutumiya bila ubaguzi na kushirikisha kila mtu;

24. Kuendelea na kuimarisha ukusanyaji na habari na uchunguzi ndani ya inchi na kwenye ngazi ya kimataifa ili kuelewa gisi watoto kwenye vikundi vya kiasili, vya watu wachache na waliyo tengwa wanapelekwa mbele ya sheria, gisi wana zuwiliwa kupata haki, na sababu kubwa za tofauti mbaya kwa watoto hawa kutoka kwenye mifumo ya haki, ili kuwazuwia kuwakilishwa kupita kiasi katika mfumo na kuendeleza njia ya kushirilikia inayo eleweka, inayo faa na ya kudumu;

25. Kulinda na kuheshimu makubaliano ya juu-ya kisiasa kwa kuwezesha mifumo ya haki ya mtoto isiyo baguwa na inayo shirikisha watoto wote na kupata haki sawa kwa watoto, kwa kutumia muda na njia inayo faa, ya kutosha na yenye usawa na kutowa mafunzo kwa watowa huduma wote wanao saidiya watoto wenye kupelekwa mbele ya sheria;

## Kuwezesha watoto kupata haki wakati wa majanga na miripuko ya magonjwa

26. Kupitisha kanuni ya kisheria na ya misingi kwa ajili ya hatua za kisheriazenye ubunifu na zenye kudumu hatua kwa watoto wakati wa hali ya zarura na isiyo ya zarura ili kuwezesha watoto wote waendelea kupata haki;

27. Kuzingatia kuweka uendeshaji wa mahakama, mashtaka, mahojiano, kesi na taarifa kupitia mutandao, na hatua zingine, kwa namna ambayo inahakikisha ulinzi wa hatua, unao kamilisha usikilizaji wa mashtaka na hatua za uso kwa uso, na zinazo undwa kwa kuzingatia kanuni zilizo jaribiwa na zinazo faa, kwa kuzingatia mgawanyiko wa kidijitali na kijiografia, upatikanaji na kushirikisha watu wote, usalama na kulindwa, kulinda siri, na kiwango cha makubaliano na kujisikia muzuri kwa mtoto;

28. Kuanzisha na kutumia mbinu zinazo eleweka kwa ushirikiano wa vituo na sekta mbalimbali katika kupanga na kukabiliana na hali ya zarura/mizozo, na kuhakikisha kwamba vyombo muhimu katika mifumo ya ulinzi na haki ya mtoto vinachukuliwa kuwa huduma muhimu zinazo ruhusiwa na kuzingatiwa zaidi kwa kutumika wakati wa janga ao zarura;

29. Kujenga uwezo wa watowa huduma ya haki kwa njia ya sasa ili kuwatayarisha kupitisha na kutumia kwa haraka na kwa ubora hatua na vifaa viliyo tayarishwa na kuwekwa kwa ajili ya kukabiliana na hali mbalimbali wakati wa majanga;

30. Kutayarisha vifaa ya kutowa habari kwa watoto wote yenye kuzingatiya jinsia, na ulemavu kuhusu mbinu za kupambana na vinyume na kutokuwa na uhakika kutokana na hali ya majanga na miripuko ya magonjwa kuhusiana na haki za watoto na fursa za kupata haki;

## Kuwezesha watoto wote wenye kupelekwa mbele ya sheria kupata haki

31. Kufwatilia mbinu tofauti katika kupata haki kwa watoto, kulingana na uongozi bora kati ya sekta na kati ya washirika, kwa njia inayo punguza hali ya kupeleka watoto mbele ya sheria kwa makosa isiyo faa;

32. Kutowa haki, huduma za kijamii, habari na musaada wowote wa kisheria ao usiyo wa kisheria unao faa kwa watoto wote wenye kupelekwa mbele ya sheria kwa kuzingatiya jinsia, aina yoyote ya ulemavu, habari kuhusu afya ya akili kwa njia yoyote, katika namna

inayo jibiya kwa mahitaji binafsi, kitambulisho, kwenye anatokeya, hali na kukomala kwa mtoto;

33. Kuhakikisha watoto ambao wanapelekwa mbele ya sheria wanapata musaada wa afya ya akili  na kisaikolojia na familia zao ziweze kupambana, kuzowea, na kubadilika ndani ya hali za kipekee zenye zinapatikana  ;

34. Kutambuwa na kuweka mbinu bora za kutatuwa, kuimarisha na kusaidia jamaa, na kuendelea kuimarisha na kutowa mafunzo kwa jamii kwa njia ya kuimarisha mipango ya ulinzi wa jamii na huduma, ili kukata njia na hali zinazo sababisha watoto kupelekwa mbele ya sheria, kuzuwia na kupunguza hatari zinazo weza kusababisha tabia ya kukera ao kukera kwa mara ya pili, na kuwezesha watoto kuishi utoto wa kawaida bila kunyanyaswana kupatikana katika hali ya shida;

35. Kuzingatiya zaidi kurudisha haki, kubalisha mawazo na kuwarudisha watoto wote wanao pelekwa mbele ya sheria katika hali mupya kupitia mbinu zinazo eleweka, kutayarishwa na kulenga namna ya kuendesha mashtaka , kuliko njia za kijumla zenye kutenga wanao husika;

36. Kutohukumu tabia ya mtoto ambayo inapashwa na inaweza kushurulikiwa kwa namna bora zaidi kwa mfano na mifumo inayo husika na ulinzi wa mtoto, ulinzi wa kijamii, huduma ya afya, afya ya akili na musaada wa kisaikolojia, ikiwemo suluhisho mbalimbali kwa makosa inayo husiana na madawa ya kulevya na kuondolewa kwa makosa ya hali; na

37. Kuanzisha mafunzo ya kipekee, kurekebisha mafunzo ya kitaalamu, na kuendelesha namna mupya ya kutowa huduma kwa ajili ya kutayarisha kazi zenye uwezo na ushindani kwenye karne ya 21 kuhusu haki ya mtoto na wale wanao husika katika ulinzi wa mtoto wasaidizi na watowa huduma, hasa watowa huduma ya kisheria, maafisa wa kutekeleza sheria, waendesha mashtaka, maafisa wa mahakama, maafisa wa kurekebisha makosa na wafanyakazi wahuduma za kijamii, kuhusu mada zikiwemo za maendeleo ya mtoto, mbinu za kuhoji na kuuliza zinazo faa kwa watoto, hatua zinazo faa za kuzuwia hali ya kusababisha tena shida ya kiakili na mbinu za kupunguza kwa uangalifu upendeleo.

Waundas heria

**Mpango wa Kimataifa wa Haki kwa Watoto** ni mpango wa pamoja uliyo tayarishwa na muungano wa mashirika ya kimataifa ambayo inatayarisha Mikutano ya Dunia kama Hatua ya Kimataifa ya Haki ya Watoto na pia hushirikisha na kuhimiza miungano ya kimataifa ya watowa huduma ya haki kupitiya Haki ya Watoto kwa njia ya mtandao. Inalenga kurahisisha mazungumuzo muhimu na kutatuwa matatizo miongoni mwa wataalamu kwa njia ya mtandao na fasi kwa ajili ya kubalishana mawazo, kuzungumuza na kujifunza mara kwa mara kuhusu haki ya mtoto.

Mikutano **ya Dunia kuhusu haki kwa watoto** zina tayarishwa kwa ajili ya kutatuwa zaidi shida za sasa kuhusu watoto wenye kupelekwa na/ao wenye kuwa na makosa mbele ya sheria, na inatowa nafasi nzuri kwa watoto na vijana, watunga sheria na watowa huduma za kisheria, wasomi, shirika ya kiraia na wawakilishi wa Umoja wa Mataifa, na wajuzi wa mambo na watowa huduma wengine: (1) Kuhimiza mifumo ya haki bora na inayo faa kwa ajili na kwa watoto duniani kote; (2) Kutowa nafasi kwa wataalamu kubadilishana njia bora, kukuza ushirikiano wa kisayansi, kutunga mapendekezo ya mbinu, na kuongeza uhimizaji kuhusu haki kwa watoto; na (3) Kusaidiya utumiaji wa vifaa vya sheria kwa ngazi ya kimataifa kuhusu haki za watoto na vijana wenye wanapelekwa mbele ya sheria.

Mkutano ya Dunia ya **2021 kuhusiana na Haki kwa watoto** ililenga kubadilishana mawazo juu ya mbinu zinazo zingatia mifano ili kupunguza ubaguzi ambayo ina sababisha mifumo ya haki kutotumia - na kutokuwa na ubora - na kuhakikisha watoto wote wanapata haki sawasawa mbele ya sheria. Washiriki kwenyemikutano iliyo fanyika kwa ngazi ya kimataifa na ya kanda na mikutano ndogo yenye kulenga suluhisho ikiwemo mazungumuzo inayo endeshwa na wataalamu, mafunzo zilizo hakikishwa na mikutano ya vikundi ambazo zinazingatia mbinu. Katika mada ya jumla ya "Kuhakikisha watoto wote kutumia chombo cha haki: kuelekea mifumo ya haki ya mtoto isiyo na ubaguzi na inayo shirikisha watu wote", mada ndogo 11 zilizingatiwa zaidi wakati wa Mkutano wa Dunia:

- Ubaguzi wa rangi na hukumu ya makosa isiyo lingana ya watoto kutoka kwenye makundi ya kiasili, kikabila na vingine vikundi vyenye watu wadogo;
- Ubaguzi kutokana na jinsia, mwelekeo wa kingono, na utambulisho wa kijinsia: kukuza mbinu ya haki ya kijisia;
- Ubaguzi kwa watoto na vijana waliyo hama maeneo yao ikiwemo wakimbizi, watoto wa kigeni wasiyo na walezi, na watoto wa wazazi wa kigeni;
- Ubaguzi kutokana na ulemavu na hali ya afya;
- Ubaguzi kutokana na matumizi ya madawa ya kulevya na unyanyasaji;
- Kuhukumu makosa kutokana na tabia za watoto kwenye mitandao;
- Umri wa miaka na makosa ya hali;
- Kuhakikisha kwamba sauti ya mtoto inasikika katika mifumo ya haki ya mtoto;
- Kutimiza haki za watoto katika hali ya uwingi wa sheria;
- Kujenga mifumo bora ya haki ya mtoto wakati wa majanga na miripuko ya magonjwa; na
- Kupambana na unyanyasaji ndani ya mifumo ya haki ya mtoto na kuhakikisha mbinu zoevu kwa watoto kwa wahanga, wenye makosa na mashahidi.

Hii **Makubaliano ya Kimataifa kuhusu Haki kwa Watoto** ilitayarishwa na Muungano wa Mkutano wa Dunia na Kundi lake la Ushauri la Watoto na Vijana, pamoja na maoni kutoka kwa Kamati ya Kisayansi, washirika watayarishaji na washiriki kwenye Mkutano wa Dunia na mikutano yake ya matayarisho.

Kwa maelezo zaidi, tembelea www.justicewithchildren.org.